# NISHATI

HABARI ZA NISHATI

# News Bulletin

www.nishati. go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati

Toleo Namba 14 — Mei 1-31, **2020**



# MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE HAUJAWAHI KUSIMAMA – WAZIRI KALEMANI



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mwenye shati la bluu) na Ujumbe wake, akiteremka kutoka katika Mashine maalumu ya kutengeneza kokoto zitakazotumika katika ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP). Waziri alikuwa katika ziara ya kazi kukagua maendeleo ya Mradi huo, Aprili 5, 2020.*

## GGM kutumia umeme wa Gridi ya Taifa Juni 2020

UK. 6




**JARIDA HILI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au

**Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma**



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akisikiliza maelezo kutoka kwa Msimamizi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), Mhandisi Steven Manda (wa pili kutoka kulia), kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi huo, Aprili 5, 2020.*

# MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE HAUJAWAHI KUSIMAMA – WAZIRI KALEMANI

**Veronica Simba – Pwani**

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani amekagua Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) kwa mara ya 11 tangu kuanza utekelezaji wake na kukiri kuridhishwa na maendeleo yake.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea sehemu mbalimbali za Mradi huo ulioko Rufiji mkoani Pwani, Aprili 5 mwaka huu, Dkt Kalemani amewataka Watanzania kuiamini Serikali na kuondoa hofu kuhusu ukamilikaji wake kwa wakati.

"Napenda niwatoe hofu Watanzania kuwa, Mradi huu haujawahi kusimama, hautasimama na utakamilika kwa wakati kama Serikali ilivyoahidi."

Waziri alikuwa akijibu swali la mmoja wa waandishi aliyetaka kufahamu kuhusu tetesi kutoka kwa baadhi ya watu kuwa huenda Mradi huo usikamilike kwa wakati.

Akieleza kwa kina kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi husika, Dkt Kalemani alibainisha kuwa kwa ujumla maendeleo ni mazuri kwani tathmini inaonesha kuwa kwa kazi za msingi, ujenzi umefikia asilimia 78.

Alifafanua kazi hizo kuwa ni pamoja na ujenzi wa njia ya kupokelea umeme (switch yard) ambayo hadi sasa Mkandarasi ametekeleza kulingana na mpango-kazi.

Nyingine ni ujenzi wa eneo ambalo maji yataingia kwa ajili ya kupelekwa kwenye mitambo (wáter in-take) ambalo nalo utekelezaji wake hadi sasa unaendana na mpango-kazi wa mkandarasi.

"Hata hivyo, katika eneo hili, kwenye kingo za maji kuna shida kidogo kwa sababu maji ni mengi, hivyo nimemwagiza Mkandarasi kuongeza kasi pindi maji yatakapopungua ili afidie muda na hivyo hali hiyo isiathiri ukamilishaji kazi husika kwa wakati uliopangwa," alieleza Waziri.

Alielezea kazi nyingine aliyokagua kuwa ni eneo lililojengwa mitambo ya kusaga mawe kwa ajili ya kokoto za ujenzi ambapo alibainisha kuwa kazi husika imekamilika kwa asilimia 100.

Vilevile, Waziri alibainisha kuwa amekagua eneo ambako zitafungwa mashine tisa kwa ajili ya kufua umeme na kubaini kuwa kazi ya ujenzi katika eneo hilo hadi sasa imetekelezwa kwa kiasi kinachozidi kile kilichoainishwa katika

INAENDELEA UK. 4


NISHATI HABARI ZA NISHATI
News Bulletin
Toleo Namba 14
Mei 1-31, 2020
MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE HAUJAWAHI KUSIMAMA – WAZIRI KALEMANI
GGM kutumia umeme wa Gridi ya Taifa Juni 2020
JARIDA HILI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI

**Mhariri**
**Veronica Simba**
(Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini)

**Waandishi**
**Veronica Simba**
**Teresia Mhagama**
**Zuena Msuya**
**Hafsa Omar**

**Msanifu Kurasa**
**Lucas Gordon**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148 au

**Fika Ofisi ya Mawasiliano**
Mtumba Dodoma, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma

*www.nishati. go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*

# EWE MDAU WA NISHATI CHUKUA TAHADHARI DHIDI YA CORONA

Kwenu wasomaji na wadau wetu wa sekta ya nishati. Leo, tunawiwa kuzungumzia janga hili la kimataifa la ugonjwa wa Corona (COVID-19) ambalo linaendelea kuitesa Dunia.

Kupitia jukwaa hili, tunawakumbusha na kuwasisitiza kufuata maelekezo yote yanayoendelea kutolewa na viongozi wetu wakuu wa serikali pamoja na wataalamu wa afya katika kujikinga na janga hili.

Tumewiwa kusisitiza hili kutokana na utafiti usio rasmi, ambao unaonesha kuwa wako baadhi ya wananchi ambao bado wanapuuza ama hawalichukulii kwa uzito unaostahili janga hili hivyo hawatekelezi ipasavyo maelekezo yanayotolewa na mamlaka husika.

Kuna msemo maarufu wa wahenga usemao "Asiye sikia la mkuu huvunjika guu" na mzaha mzaha hutumbuka usaha!!" Ugonjwa wa COVID -19 upo na kamwe tusichukulie mzaha!! Tunayo mifano ya nchi kama Italia na Uhispania ambazo wakati ugonjwa huu umeingia katika nchi ya China, hawakulichukulia janga hilo kwa uzito unaostahili na matokeo yake sasa nchi hizo ni miongoni mwa zinazoongoza kwa maambukizi.

Tunapenda kuwaarifu kwamba Wizara ya Nishati inalichukulia kwa uzito wa hali ya juu janga hili na tayari inatekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na viongozi wakuu wa serikali pamoja na wataalamu wa afya.


Aidha, katika kuhakikisha Taasisi zilizo chini ya Wizara pia zinatekeleza maagizo hayo ipasavyo, viongozi wa Wizara wamekuwa wakitembelea na kufanya ukaguzi katika ofisi mbalimbali za Taasisi.

Hivi karibuni Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu alitembelea Ofisi za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Morogoro na kupongeza hatua ambazo shirika hilo limekuwa likichukua katika kuhakikisha linawakinga watumishi na wateja wake dhidi ya ugonjwa huo kadri ya uwezo wake.

Jitihada hizi zote zinazofanywa na Wizara hazitakuwa na maana na hazitazaa matunda pasipo ninyi wadau wetu kutoa ushirikiano. Hivyo basi, tunategemea kuanzia sasa, kwa wale ambao walikuwa hawalichukulii suala hili kwa uzito, wataanza kufanya hivyo.

Hata hivyo, kama ambavyo Mheshimiwa Rais wetu John Pombe Magufuli ametuasa pia, pamoja na kuchukua tahadhari kadri tunavyoelekezwa lakini pia tusisahau kumwomba Mungu, kila mmoja kwa imani yake ili atuepushe na janga hili.

Sote tukitimiza wajibu wetu pamoja na kumwomba Mungu, bila shaka atatuepusha na janga la CORONA.



# Katunika Ki-nishati



# MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE HAUJAWAHI KUSIMAMA – WAZIRI KALEMANI

INATOKA UK. 2

mpango-kazi kwa siku takribani 30.

Aidha, Dkt Kalemani alikagua pia kituo cha Reli ya TAZARA cha Fuga ambacho ni maalumu kwa kushushia mitambo yenye uzito mkubwa inayotumika katika ujenzi wa Mradi. Akiwa eneo hilo, Waziri alishuhudia mizigo ikishushwa na kupelekwa eneo la Mradi.

"Naipongeza Serikali kwa kujenga Reli hii na kuweka Kituo rasmi kwa ajili ya kushusha mizigo ya Mradi huu. Hii inawezesha kazi za Mradi huu kuendelea kama kawaida pamoja na changamoto ya mvua zinazoendelea kunyesha nchini.

Hata hivyo, Waziri Kalemani alitoa wito kwa watendaji wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), kuijenga kwa kiwango cha lami, barabara kutoka kituo cha Reli cha Fuga hadi eneo la Mradi, umbali wa kilomita 35.8 ili iwe katika viwango bora zaidi kuwezesha usafirishaji wa mizigo mizito ya Mradi.

Waziri pia alikagua barabara zote zilizo ndani ya eneo la Mradi na kuthibitisha kuwa zinapitika vizuri. Alitoa wito kwa Mkandarasi kuendelea kukarabati maeneo korofi ya barabara hizo ikiwa ni pamoja na zile zilizo nje ya Mradi, hususan zilizo ndani ya wajibu wake ili ziendelee kutumika kusafirisha mizigo na wafanyakazi pasipo tatizo lolote.

Akizungumzia malipo kwa Mkandarasi, Dkt Kalemani alipongeza Serikali kwa kulipa jumla ya shilingi trilioni 1.19 kati ya trilioni 6.5 za malipo yake yote, ambayo ni sawa na asilimia 18.8 huku akibainisha kuwa kiwango hicho ndicho stahili iliyopaswa kulipwa kufikia wakati huu, hivyo Mkandarasi hana kisingizio cha kutotekeleza majukumu yake.

Katika hatua nyingine, Waziri aliushukuru Uongozi wa Mikoa ya Morogoro na Pwani kwa kuendelea kutoa ushirikiano katika usimamizi wa Mradi.

Hata hivyo alitoa wito kwa Mikoa inayohusika na vyanzo vya maji yatakayotumika katika Mradi huo, kuhakikisha kuwa pamoja na matumizi ya maji katika shughuli zao za kiuchumi lakini wananchi wake wanapaswa kuhakikisha matumizi hayo hayaathiri upatikanaji wa maji kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi.

Aliitaji mikoa hiyo kuwa ni pamoja na Morogoro, Njombe, Iringa na Mbeya.

"Bwawa hili litakapokamilika litahitaji maji mengi kiasi cha mita za ujazo bilioni 32.3 hivyo nawasihi sana wananchi wa Mikoa husika kutoathiri upatikanaji wake," alisisitiza Waziri.

Vilevile, Dkt Kalemani alitoa maelekezo kwa Uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kuanza taratibu za kumpata Mkandarasi atakayejenga njia ya kusafirisha umeme kutoka eneo la Mradi hadi Kinyerezi jijini Dar es Salaam, umbali wa kilomita 167 ili kuuingiza kwenye gridi ya Taifa.

"Nataka Mradi huu unapokamilika na njia ya kusafirisha umeme huo iwe imekamilika tayari kwa kuanza kuusafirisha na kuuingiza kwenye gridi ya Taifa."

Katika ziara hiyo, Waziri alifuatana na viongozi mbalimbali wa Serikali pamoja na wataalamu akiwemo Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt Tito Mwinuka, Meneja wa Shirika hilo mkoani humo, Mhandisi FedGrace Shuma, Mwakilishi wa Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Ahmed Chinemba pamoja na wataalamu wengine mbalimbali.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mwenye miwani) na Ujumbe wake, wakiangalia shehena ya nondo zenye uzito wa tani 2,000 zilizoagizwa na Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) kutoka nje ya nchi na kupigwa marufuku na Serikali kuzitumia ambapo ametakiwa atumie vifaa vya ndani ya nchi. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi kukagua maendeleo ya Mradi huo, Aprili 5, 2020.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa pili kutoka kushoto), akitoa maelekezo kwa Msimamizi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), Mhandisi Steven Manda (kulia), alipokuwa akikagua zoezi la kushushwa mizigo mizito kwa matumizi ya Mradi, katika Kituo cha Reli ya TAZARA cha Fuga, Aprili 5, 2020.*

# MATUKIO PICHANI









*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake, wakikagua maendeleo ya Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), Aprili 5 mwaka huu.*





*Hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), wakati Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) alipotembelea Mradi huo Aprili 5, 2020 kwa mara ya 11 tangu kuanza kutekelezwaji wake.*

# GGM kuanza kutumia umeme wa Gridi ya Taifa Juni mwaka huu

*Zuena Msuya - Geita*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medrad Kalemani (katikati) akitoa maelekezo kwa wakandarasi wanaotekeleza ujenzi wa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Mponvu mkoani Geita baada ya kuridhishwa na kasi ya ujenzi wa kituo hicho alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho hivi karibuni.*

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amesema kuanzia Juni mwaka huu, Mgodi wa kuchimba dhahabu wa Geita (GGM) utaanza kutumia umeme wa Gridi ya Taifa kuendesha shughuli zake baada ya Kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Mponvu mkoani Geita kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2020.

Aidha, alisema ameridhishwa na kasi ya ujenzi wa kituo hicho ambacho awali kilipangwa kukamilika mwezi Juni lakini kutokana na kasi ya ujenzi wake kitakamilika mwishoni mwa Mwezi Mei na kuanza kusambaza umeme kwa wateja ikiwemo GGM.

Dkt. Kalemani alisema hayo, alipofanya ziara ya kikazi Aprili 25, 2020, mkoani Geita kukagua ujenzi wa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Mponvu, Kituo cha kuchenjua dhahabu cha Geita na kuwasha umeme katika Kijiji cha Buyagu na Zahanati ya Musasa.

"kituo hiki cha Mponvu kitakuwa mkombozi mkubwa wa nishati ya umeme wa kutosha na kwa gharama nafuu, kwa wakazi wa Mkoa wa Geita na mikoa jirani. Pia, Mgodi wa GGM utajiendesha kwa faida zaidi na kuliongezea mapato taifa kwa sababu wataacha kutumia jenereta kuzalisha umeme ambao ni wa gharama kubwa sana ukilinganisha na umeme unaozalishwa hapa nchini," alisema Dkt. Kalemani.

Alifafanua kuwa, mgodi wa GGM utatumia umeme wa gridi ya taifa kutoka kituo cha Mponvu ambacho kitapokea umeme kupitia njia ya kusafirisha umeme wa Kilovolti 220 kutoka kituo cha Bulyanhulu mkoani Shinyanga hadi mkoani Geita yenye urefu wa kilomita 55.

Vilevile, alieleza kuwa tayari njia ya kusafirisha umeme wa Kilovolti 33 utakaotumiwa na mgodi huo, yenye urefu wa Kilomita 6.5 kutoka katika kituo hicho hadi ndani ya mgodi huo imekamilika na kinachosubiriwa sasa ni kuunganisha umeme punde kituo hicho kitakapokamilika.

Dkt. Kalemani pia aliwasha umeme katika Kijiji cha Buyagu, ambacho ni moja ya vijiji vinavyopitiwa na njia ya kusafirisha umeme wa Kilovolti 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita ikiwa ni ishara ya kukamilika kwa njia hiyo kwa asilimia 80.

Katika kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini, aliwasha umeme katika zahanati ya Musasa na kuwataka wananchi wa eneo hilo kuendelea kulipia ili waunganishiwe umeme.

Katika hatua nyingine, aliliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuharakisha ufungaji wa Mashineumba (Transfoma) katika kituo cha kuchenjua dhahabu mkoani Geita ambacho kiko katika hatua za mwisho kukamilika.

Dkt. Kalemani alirejea kusema kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa wachimbaji wote wa madini wanaendesha shughuli za uchimbaji kwa kutumia nishati ya umeme unaozalishwa nchini kwa gharama nafuu.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel alisema kuwa kituo hicho kikikamilika kitakuwa na uwezo wa kuchenjua dhahabu inayotakiwa katika ubora wa kimataifa na kitawasaidia wachimbaji wadogo kunufaika zaidi na shughuli zao za uchimbaji tofauti na ilivyo sasa.

Gabriel aliwaomba wawekezaji kwenda kuwekeza zaidi katika Mkoa huo wa Geita kwa kuwa kuna umeme mwingi, wa kutosha na wenye gharama nafuu kuendesha shughuli mbalimbali vikiwemo viwanda.

Vilevile aliishukuru Wizara ya Nishati kwa kuhakikisha kuwa Mkoa huo unakuwa na umeme wa kutosha ili kuvutia wawekezaji wengi pamoja na kuwaunganishia umeme wa bei nafuu wananchi wa Mkoa huo na kujengwa kwa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Mponvu ambacho kitawezesha migodi yote katika Mkoa husika kutumia umeme, na kuugawa katika mikoa jirani.

# MATUKIO PICHANI



Mwonekano wa sehemu ya mitambo iliyopo katika kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Mponvu kinachotarajiwa kukamilika mwishoni mwa Mwezi Mei, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akikagua mashine zilizofungwa ndani ya jengo la kuendeshea mitambo (Control Room) katika Kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Mponvu mkoani Geita baada ya kufanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho hivi karibuni.



Mwoneko wa jengo la kuendesha mitambo (Control room) katika Kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Mponvu mkoani Geita.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kushoto) na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel (kulia) wakipita katika tope wakati wakikagua eneo la ujenzi wa kituo cha kuchenjua dhahabu cha Geita pasipo kujali mvua kubwa iliyokuwa ikinyesha.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kushoto) akizungumza na baadhi ya viongozi wa kijiji cha Buyagu (hawapo pichani) akiwataka wakawahamasishe wananchi wao kulipia gharama za umeme ili waunganishiwe huduma hiyo. Waziri aliwasha umeme katika kijiji hicho. Katikati ni Mbunge wa Busanda, Lolensia Bukwimba



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (katikati), Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel (kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Geita, Josephat Maganga (kushoto) wakiwa katika eneo linalojengwa jengo la utawala katika eneo la uwekezaji mkoani Geita.

# NAIBU WAZIRI MGALU AMTAKA MKANDARASI KUMALIZA KAZI KWA WAKATI

***Na mwandishi wetu – Morogoro***

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, amefanya ziara mkoani Morogoro na kumwagiza Mkandarasi, Kampuni ya State Grid, anayetekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, mkoani humo kumaliza kazi kwa wakati.

Mgalu alilazimika kufanya ziara hiyo baada ya kupokea malalamiko ya kusuasua kwa Mradi husika ambapo aliwaagiza watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kumsimamia Mkandarasi huyo ili kuhakikisha anakamilisha kazi kwa muda ulioainishwa kwenye Mkataba.

Wakati wa ziara hiyo iliyofanyika Aprili 25 mwaka huu, Naibu Waziri alitembelea baadhi ya vijiji vya Wilaya za Gairo na Mvomero kujionea maendeleo ya kazi husika.

Vijiji vilivyotembelewa ni Ukwamani na Nguyami (Gairo) pamoja na Komtanga (Mvomero). Kadhalika, Naibu Waziri alitembelea Yadi ya Mkandarasi iliyopo Gairo Mjini.

Naibu Waziri aliwaasa viongozi na wananchi wote kwa ujumla kuendelea kuchukua tahadhari juu ya ugonjwa wa Covid – 19 unaosababishwa na virusi vya Corona huku wakiendelea kufanya shughuli zao.

Pia, aliwataka TANESCO Mkoa wa Morogoro kuhakikisha wananchi wote wanaolipia ili kuunganishiwa umeme, wanapatiwa huduma hiyo kwa wakati.



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (katikati-mwenye ushungi), akikagua kazi ya kuunganisha umeme vijijini inayoendelea katika eneo la Ukwamani, wilayani Gairo hivi karibuni.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (mwenye ushungi), akikagua Yadi ya Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, wilayani Gairo, akiwa katika ziara ya kazi hivi karibuni.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (kushoto), akikagua maendeleo ya kazi ya usambazaji umeme vijijini katika kijiji cha Komtanga, wilayani Gairo, akiwa katika ziara ya kazi, Aprili 25 mwaka huu.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akiwasha umeme katika Zahanati ya Kijiji cha Mghamo, Singida Vijijini, Aprili 18, 2020 akiwa katika ziara ya kazi.*

# CORONA ISIWE KISINGIZIO CHA KUKWAMISHA MIRADI YA UMEME - KALEMANI

**Veronica Simba – Singida**

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani amekagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme mkoani Singida huku akitahadharisha kuwa uwepo wa janga la Corona (COVID 19) nchini usitumike kama kisingizio cha kukwamisha miradi hiyo.

Akizungumza kwa nyakati tofauti akiwa katika ziara hiyo, Aprili 18 mwaka huu, Dkt Kalemani alisisitiza kuwa ni lazima watekelezaji wa miradi husika kufuata maelekezo ya Rais John Magufuli na wataalamu wa afya katika kujikinga na Corona lakini ni lazima pia kuendelea na kazi.

"Corona ipo, ni lazima tuchukue tahadhari zote za kujikinga kama tunavyoelekezwa lakini kwa upande mwingine maisha inabidi yaendelee hivyo tunawajibika kuendelea kufanya kazi."

Akieleza kwa kina dhamira ya ziara yake, Dkt Kalemani alisema yeyé pamoja na viongozi wenzake wa sekta ya nishati, wanalazimika kufanya ziara hizo ili kuhakikisha wakandarasi na wasimamizi wa miradi husika hawabweteki na kutelekeza kazi hususan katika kipindi hiki cha janga la Corona.

Akifafanua zaidi, alisema hakuna anayejua janga hilo litaisha lini hivyo ni lazima kuendeleza mapambano kwa kufanya kazi maana Watanzania wangali wanahitaji umeme.

Hata hivyo, Waziri Kalemani alikagua miradi husika kwa utaratibu tofauti na uliozoeleka ambapo haukuhusisha mikusanyiko ya wananchi badala yake walioshiriki ni viongozi pekee wa ngazi za wilaya, kata, vijiji na vitongoji.

Aliwataka wananchi kubaki majumbani na kwamba watapata maelekezo ya Serikali kupitia kwa viongozi wao na katika vyombo vya habari.

"Nilitoa maelekezo kuwa katika kipindi hiki cha janga la Corona, ziara zetu zitahusisha viongozi peke yake ili kuepusha mikusanyiko ya watu, ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo tuliyopatiwa na wataalamu wa afya katika kujikinga na ugonjwa huu.

Katika ziara hiyo, Waziri aliagiza kusakwa na kukamatwa Mkandarasi Emmanuel Nyigwa, anayedaiwa kuchukua pesa za wananchi kwa makubaliano ya kufanya kazi ya kusuka mfumo wa nyaya za umeme (wiring) katika nyumba zao lakini akatoweka pasipo kufanya kazi hiyo.

Aidha, kufuatia malalamiko hayo yaliyowasilishwa kwake na Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, Waziri alitoa maelekezo kwa mameneja wote wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) nchi nzima, kuchukua dhamana ya kuwasajili kwa kuwagongea muhuri wakandarasi wanaofaa kufanya kazi ya kusuka mfumo wa nyaya katika majengo ili kuwaepusha wananchi na adha kama hiyo iliyotokea.

Alisema uthibitisho huo wa Meneja husika utamaanisha kuwa taarifa zote za Mkandarasi ikiwemo namba zake za simu na mahali anakoishi zinafahamika na kurekodiwa ili kuwa na uhakika wa kumpata pindi anapokiuka makubaliano.

Katika hatua nyingine, Waziri alikagua kazi inayoendelea ya upanuzi wa Kituo cha kufua umeme cha Singida, ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi mkubwa wa umeme ujulikanao kama Backbone Transmission Investment Project (BTIP) Awamu ya Pili.

Aliagiza kazi hiyo ikamilike ifikapo Julai mwaka huu kama yalivyo makubaliano na kusisitiza kwamba kamwe Serikali haitaongeza muda kwakuwa ilikwishafanya hivyo awali.

Waziri pia aliwasha umeme katika maeneo mbalimbali ikiwemo vituo vya afya, sehemu za biashara na makazi ya wananchi katika vijiji vya Nkuhi, Muungano, Matare na Mghamo katika Wilaya za Ikungi na Singida Vijijini.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, viongozi mbalimbali akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Ikungi Edward Mpogolo, Mbunge wa Singida Mashariki Miraji Mtaturu na Mbunge wa Singida Kaskazini Justin Nonko, walipongeza jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Wizara ya Nishati, katika kuwapelekea wananchi huduma ya umeme hususan vijijini.

Waziri anatarajiwa kuhitimisha ziara yake mkoani humo, Aprili 20, mwaka huu.

# MATUKIO PICHANI



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mwenye kipaza sauti), akizungumza na viongozi wa Kijiji cha Matare na vitongoji vyake, baada ya kuwasha rasmi umeme katika Zahanati ya Kijiji hicho kilichopo wilayani Ikungi, Mkoa wa Singida, Aprili 18, 2020. Utaratibu wa sasa wa Waziri akiwa ziarani ni kuzungumza na viongozi pekee ili kuepusha mikusanyiko mikubwa ya wananchi, ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya wataalamu wa afya katika kujikinga na janga la ugonjwa wa Corona.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati) akizungumza na viongozi wa kijiji cha Nkuhi, Kata ya Isuna, wilayani Ikungi, Mkoa wa Singida (hawapo pichani), baada ya kuwasha umeme katika nyumba ya Mzee Gabriel Alute (hayupo pichani), Aprili 18 mwaka huu. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogolo na kushoto ni Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu.*



*Mafundi wakiendelea na kazi za ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Singida. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), Aprili 18, 2020.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akitakasa mikono kwa kunawa alipowasili katika Zahanati ya Kijiji cha Mghamo, Singida Vijijini ambapo aliwasha rasmi umeme akiwa katika ziara ya kazi, Aprili 18 mwaka huu.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake, wakikagua maendeleo ya ujenzi unaolenga kupanua Kituo cha kupoza umeme cha Singida, akiwa katika ziara ya kazi Aprili 18, 2020.*



*Viongozi wa kijiji cha Mutare, wilayani Ikungi, Mkoa wa Singida, wakiwa wamesimama kwa kuachiana nafasi ili kuchukua tahadhari dhidi ya Corona, wakati wakimsikiliza Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), katika tukio la kuwasha umeme katika Zahanati ya kijiji hicho, Aprili 18 mwaka huu.*

# MATUKIO PICHANI



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa tatu kutoka kulia), akikata utepe kabla ya kuwasha rasmi umeme katika Zahanati ya Mutare, wilayani Ikungi, Mkoa wa Singida akiwa katika ziara ya kazi, Aprili 18 mwaka huu. Kushoto kwake ni Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogolo na kulia kwa Waziri ni Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu.*










# Bodi ya TGDC yaridhishwa na mradi wa jotoardhi Songwe



Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi kutoka Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), Taramaeli Mnjokava akitoa ufafanuzi mbele ya Bodi ya TGDC katika eneo la Mradi wa jotoardhi wilayani Mbozi mkoani Songwe. Kutoka kulia ni Mwenyekiti wa Bodi hiyo Beatus Segeja, Mjumbe wa Bodi Elisante Mshiu, Mjumbe wa Bodi Tito Mwinuka na Meneja Mkuu wa TGDC Mhandisi Kato Kabaka.

**Augustino Kasale - Songwe**

Bodi ya Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) imeelezwa kuwa TGDC imekamilisha taratibu za upatikanaji eneo la uendelezaji miradi ya jotoardhi wilaya ya Mbozi mkoani Songwe.

Hayo yamesemwa na Meneja Mkuu wa TGDC, Mhandisi Kato Kabaka wakati wa ziara ya Bodi hiyo iliyolenga kukagua miradi ya jotoardhi wilayani humo hivi karibuni.

"Hatua tuliyofikia ni nzuri kwani mpaka sasa tumefanikiwa kupata eneo lenye ukubwa wa kilomita za miraba 18.59," alisema Mhandisi Kabaka.

Aidha, Mhandisi Kabaka alifafanua kuwa eneo hilo litatumika kwa ajili ya miradi ya jotoardhi ya moja kwa moja ikiwa ni pamoja na miradi ya kilimo cha kutumia nishati ya jotoardhi na mradi wa utalii unaohusisha kujenga miundombinu itakayotumia jotoardhi.

Aliainisha kuwa, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo ni utangazaji wa zabuni ili kupata wakandarasi watakaotekeleza shughuli zilizoko katika miradi hiyo.



Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi kutoka Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), Taramaeli Mnjokava akimwelekeza Mwenyekiti wa Bodi ya TGDC Beatus Segeja mipaka ya eneo la Mradi wa jotoardhi lililoko wilayani Mbozi. Kushoto ni Meneja Mkuu wa TGDC Mhandisi Kato Kabaka.

"Pamoja na uendelezaji wa shughuli nilizozitaja, kampuni inalenga kuboresha miundombinu ya barabara kuhakikisha eneo la mradi linafikika kwa urahisi wakati wa ujenzi na mara baada ya ujenzi kukamilika," aliongezea Mhandisi Kabaka.

Vilevile, alisema kuwa toka mwanzo wa Mradi, wanakijiji wa Nanyala wamekuwa na ushirikiano wa kutosha mpaka kuwezesha kupata eneo hilo, huku Uongozi wa Wilaya na Mkoa nao ukipokea Mradi vizuri.

Aliongeza kuwa, katika Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia jotoardhi, tafiti za awali zimekamilika na kwamba hatua itakayofuata ni uchorongaji wa visima vya majaribio ili kuhakiki kiwango cha hifadhi ya nishati ya jotoardhi iliyoko chini ya ardhi kama itatosheleza kuzalisha umeme.

"Mipango tuliyonayo ni kuhakikisha eneo hili la jotoardhi linakuwa na shughuli nyingi zinazohusisha matumizi ya nishati ya jotoardhi ili kochochea shughuli za kiuchumi katika ukanda huu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya TGDC, Beatus Segeja alisema kuwa hatua iliyofikiwa katika Mradi huo ni kubwa.

"Mpaka kufikia hatua ya upatikanaji wa eneo hili ni kweli jitihada kubwa zimefanywa na kampuni," alisema Segeja.

Segeja amewataka watendaji kuongeza jitihada katika utekelezaji wa Mradi huo ili mipango ya kampuni katika eneo hilo itekelezwe kwa wakati kadri kampuni ilivyojipangia.

Alipongeza kampuni kwa ushirikiano wake na jamii inayozunguka Mradi pamoja na Uongozi wa Mkoa kwa ujumla, huku akiomba kuendeleza jitihada zaidi za kushirikisha wadau mbalimbali katika miradi ya jotoardhi.

# WAZIRI KALEMANI AFANYA ZIARA YA KUSHTUKIZA KITUO CHA KUPOZA UMEME MSAMVU

**Veronica Simba – Morogoro**

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani amefanya ziara ya kushtukiza katika kituo cha kupoza umeme Msamvu na kuagiza kazi ya kufunga kifaa cha kukata umeme (circuit breaker), ikamilishwe ndani ya siku moja ili wananchi waendelee kupata huduma ya umeme.

Alifanya ziara hiyo Aprili 4, mwaka huu akiwa ameambatana na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Dkt Tito Mwinuka, Meneja wa Mkoa wa Shirika hilo, Mhandisi FedGrace Shuma, Mwakilishi wa Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Ahmed Chinemba na wataalamu mbalimbali kutoka wizarani, TANESCO na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akimsikiliza Msimamizi wa Kituo cha Kupoza Umeme Msamvu mkoani Morogoro, Selemani Ibwe (kushoto) aliyekuwa akimpatia maelezo kuhusu hali ya kituo hicho. Wa kwanza kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt Tito Mwinuka. Waziri alitembelea kituo hicho Aprili 4 mwaka huu.*

Dkt Kalemani alitoa maagizo hayo baada ya kujulishwa kuwa changamoto ya kukatika umeme mara kwa mara ambayo wamekuwa wakiipata wananchi wa mji wa Morogoro hususan maeneo ya Mtibwa na Kilosa ni kutokana na kuharibika kwa kifaa hicho kituoni hapo hali inayowalazimu TANESCO kufunga kifaa kipya.

Waziri alitoa onyo kwa Msimamizi wa Kituo hicho, Selemani Ibwe, kuwa kosa hilo lisitokee tena kwani tayari alikwishalitolea maelekezo kwa Mameneja wa TANESCO nchi nzima.

"Hili ni onyo la mwisho kwa Mameneja wa TANESCO nchi nzima. Mnatakiwa kuhakikisha mnakuwa na vifaa vya akiba katika vituo vya kupoza umeme ili inapotokea hitilafu tatizo linarekebishwa mara moja badala ya kutumia muda mrefu na kuwasababishia kero wananchi."

Aidha, Waziri alitoa muda wa siku saba kwa wafanyakazi wawili wanaosimamia kituo hicho cha Msamvu kuhamishia makazi yao maeneo ya jirani ili waweze kushughulikia kwa wakati changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika kituo hicho.

Alisisitiza kuwa hilo pia ni onyo la mwisho kwani alikwishatoa maelekezo husika kwa watumishi wote wanaosimamia vituo vya kupoza umeme nchi nzima, kuishi katika maeneo yaliyo jirani na vituo hivyo.

Pia, Dkt Kalemani alitoa maagizo kwa uongozi wa TANESCO

INAENDELEA UK. 14



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akimsikiliza Msimamizi wa Kituo cha Kupoza Umeme Msamvu mkoani Morogoro, Selemani Ibwe (kulia) aliyekuwa akimpatia maelezo kuhusu hali ya kituo hicho. Waziri alitembelea kituo hicho Aprili 4 mwaka huu.*



*Transfoma kubwa iliyopo katika Kituo cha Kupoza Umeme Msamvu mkoani Morogoro. Taswira hii ilichukuliwa Aprili 4, 2020 wakati Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) alipotembelea kituo hicho.*

# WAZIRI KALEMANI AFANYA ZIARA YA KUSHTUKIZA KITUO CHA KUPOZA UMEME MSAMVU

INATOKA UK. 13

mkoani Morogoro kukamilisha marekebisho yanayofanyika katika njia ya kusafirisha umeme ya Mtibwa ndani ya siku tatu ili wananchi husika waendelee kupata huduma ya nishati hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari kituoni hapo, Waziri Kalemani alifafanua kuwa hali ya kukatika kwa umeme ambayo imekuwa ikitokea haisababishwi na ukosefu wa nishati hiyo bali ni kutokana na changamoto za ki-usimamizi ambazo alisema ametoa maelekezo namna ya kuzitatua.

"Mathalani hapa Morogoro umeme uliopo ni wa kutosha kwani kituo hiki kina uwezo wa kuzalisha megawati 88 wakati mahitaji ya wananchi ni megawati 48 tu," alifafanua.

Awali, kabla ya kutembelea kituo hicho, Waziri Kalemani alizungumza na waandishi wa habari akiwa katika



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mwenye miwani) akijiandaa kunawa mikono ikiwa ni kutekeleza maelekezo ya wataalamu ili kujikinga na ugonjwa wa COVID-19 alipowasili katika Kituo cha kufua umeme Msamvu, Morogoro, Aprili 4 mwaka huu akiwa katika ziara ya kazi.*

eneo la Dakawa, takribani kilomita 100 kutoka eneo kunapotekelezwa mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (megawati 2,115) ambapo alitoa maagizo kwa wakandarasi wa Mradi huo kutumia usafiri wa Reli katika kusafirisha mizigo badala ya kutegemea njia ya barabara pekee.

Huku akiwa amezingatia miongozo ya wataalamu kuhusu kutoweka mikusanyiko ya watu, Waziri alisema maelekezo hayo aliyoyatoa ni kutokana na uharibifu wa barabara husika ambao umesababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha.

"Naipongeza Serikali inayoongozwa na Rais John Pombe Magufuli kwani imejenga miundombinu mbalimbali tunayoweza kuitumia ikiwemo reli ya TAZARA badala ya kutegemea barabara pekee hali inayoweza kusababisha ucheleweshaji wa mradi."

Akisisitiza, alisema Serikali haitakubali kuona Mradi huo unacheleweshwa kwa kisingizio chochote hivyo akawataka wakandarasi husika kuendelea kuchapa kazi.

Akieleza zaidi, alisema hata yeyé msafara wake umekwama mahala hapo akiwa njiani kwenda kukagua Mradi huo lakini akasema atatumia njia mbadala kufika eneo la Mradi siku inayofuata.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Regina Chonjo ambaye alifuatana na Waziri Kalemani, alisema amewasiliana na watendaji kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ambao ndiyo wenye dhamana na barabara hiyo na kwamba wanatarajiwa kufika eneo husika kwa ajili ya kurekebisha kipande hicho ili kuwezesha magari kuendelea kupita.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt Tito Mwinuka alisema shirika lake litashirikiana na TANROADS katika kuhakikisha njia hiyo inakarabatiwa mapema na kuongeza kuwa hata Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Julius Nyerere atashirikishwa maana pia anawajibika kuchangia.





*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake wakikagua Kituo cha Kufua Umeme Msamvu, mkoani Morogoro, katika ziara ya kushtukiza, Aprili 4 mwaka huu.*

# MATUKIO PICHANI





*Malori ya mizigo yakiwa yamekwama na kuziba njia katika eneo la Dakawa, takribani kilomita 100 kutoka eneo la Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere. Taswira hii ilichukuliwa Aprili 4, 2020 wakati Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake (hawapo pichani) alipofika eneo hilo akielekea kukagua Mradi husika na kukwama.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kushoto) akipata maelezo ya ufungaji wa Mashineumba (Transfoma) katika kituo cha kuchenjua dhahabu cha Geita kutoka kwa Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Geita, Charles Msangi (katikati).*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mwenye miwani-kushoto) akizungumza na Mkazi wa Misongeni, nje kidogo ya Mji wa Morogoro, Kibena Kingo (kulia) alipopita eneo hilo akiwa katika ziara ya kazi Aprili 4 mwaka huu. Waziri aliuagiza uongozi wa TANESCO kuhakikisha nguzo za umeme zilizopo katika eneo hilo zinafungiwa nyaya na kuanza kuwaunganishia wananchi mara moja.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (mwenye ushungi), akikagua Yadi ya Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, wilayani Gairo, akiwa katika ziara ya kazi hivi karibuni.*

# WATUMISHI NISHATI WAPATA ELIMU YA CORONA



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mhandisi Zena Said (mbele) na Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Leonard Masanja (aliyekaa-kulia) pamoja na baadhi ya watumishi wa Wizara ya Nishati wakimsikiliza Mtaalamu wa Afya Jamila Hamudu (hayupo pichani), wakati akitoa elimu ya afya kuhusu ugonjwa wa Covid – 19 (Corona) katika mafunzo yaliyofanyika wizarani Aprili 15 mwaka huu.*



*Mtaalamu wa Afya, Jamila Hamudu (kushoto), akitoa elimu kuhusu ugonjwa wa Covid – 19 (Corona) kwa watumishi wa Wizara ya Nishati, hivi karibuni.*

**Hafsa Omar - Dodoma**

Watumishi wa Wizara ya Nishati wakiongozwa na Katibu Mkuu Mhandisi Zena Said na Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Leonard Masanja, wamepatiwa elimu juu ya ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya Corona na namna ya kujikinga na ugonjwa huo.

Elimu hiyo ilitolewa Aprili15 mwaka huu na Maafisa Uguuzi na Wawezeshaji wa masuala ya ugonjwa wa Covid-19 kutoka Wizara ya Afya, Jamila Hamudu na Salome Mwinjuma.

Akizungumza na wafanyakazi, Hamudu alieleza kuwa dalili za ugonjwa huo ni pamoja na homa kali, kikohozi, uchovu na kuwa na tatizo la kupumua.

Aidha, alieleza njia za kujikinga na ugonjwa huo kuwa ni pamoja na kuosha mikono mara kwa mara na maji yanayotiririka kwa kutumia sabani na vitakasa mikono (sanitizer) hata kama mikono haionekani kuwa michafu.

Alieleza sababu ya kufanya hivyo ni kwamba mtu anapoosha mikono kama inavyoelekezwa anaweza kuondoa virusi hivyo endapo viko mikononi.

Njia nyingine inayoweza kusaidia kujikinga na maradhi hayo ni kutoshika macho, pua au mdomo akisema hii ni kwa sababu mikono hushika vitu vingi ambavyo vinaweza kuwa na virusi hivyo.

Aliwataka wafanyakazi kuchukua tahadhari mbalimbali ili kujikinga na maradhi hayo ikiwa na pamoja na kuwahi hospitali ikiwa mtu atapata dalili za maradhi hayo.

Pia, aliwataka kutoa taarifa kwa vyombo husika iwapo atapatikana mgonjwa mwenye dalili za ugonjwa huo kwa kupiga namba za simu ambazo zimetolewa na Serikali.

Akifunga mafunzo hayo, Katibu Mkuu Mhandisi Said, aliwashukuru wawezeshaji hao kwa kutoa elimu ambayo itawasaidia watumishi na kuwashukuru wafanyakazi wote kushiriki kwenye mafunzo.

Aliwataka kuchukua tahadhari kama walivyoelekezwa ili kujinga wao pamoja na familia zao.





*Watumishi wa Wizara ya Nishati wakipata elimu kuhusu ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya Corona. Mafunzo hayo yalifanyika katika Ofisi za Wizara zilizopo Mtumba na Kikuyu jijini Dodoma, Aprili 15 mwaka huu.*

# Dkt. Kalemani haridhishwi na kasi ndogo ya matumizi ya umeme Tabora



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kulia) akizungumza na Mkazi wa Kijiji cha Busomeke (katikati) wilayani Igunga mkoani Tabora baada ya kuwasha umeme katika nyumba ya mwananchi huyo.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akizungumza na viongozi wa Kijiji cha Busomeke Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, alipofanya ziara ya kukagua shughuli za usambazaji umeme vijijini, Aprili 27, 2020.

**Zuena Msuya - Tabora**

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani amewataka wakazi wa Mkoa wa Tabora kuongeza kasi ya kutumia umeme unaopatikana mkoani humo kwa kuwa matumizi yao yapo chini zaidi kulinganisha na umeme unaozalishwa mkoani humo.

Dkt Kalemani alisema hayo wakati akikagua shughuli za usambazaji wa umeme vijijini katika Kijiji cha Mizanza na kuwasha umeme katika Kijiji cha Busomeke wilayani Igunga mkoani Tabora, Aprili 27, 2020.



Moja ya nyumba iliyowashiwa umeme na Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akiwa katika ziara ya kazi Kijiji cha Busomeke wilayani Igunga mkoani Tabora, Aprili 27, 2020.

Alisema kuwa, mitambo ya kufua umeme iliyopo mkoani humo ina uwezo wa kuzalisha megawati 42 za umeme ili itumike katika Mkoa mzima lakini mpaka sasa matumizi ni megawati 14 tu.

"Kwa nini ninyi wakazi wa Tabora hamtaki kutumia umeme wakati tayari miundombinu imewafikia na bei ya kuunganisha ni 27,000 tu?"

Akifafanua zaidi, Waziri alisema mitambo iliyopo Tabora ina uwezo wa kufua umeme wa megawati 42, lakini matumizi ya wananchi hayafiki hata nusu ya umeme huo.

"Hii siyo sawa. Mtaharibu mitambo yetu kwa kuwa mingine italazimika kuzimwa na ikizimwa kwa muda mrefu itaharibika na nchi itapata hasara," alisema Dkt. Kalemani.

Aliwataka viongozi wa Serikali za Vijiji, Mitaa pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuongeza kasi ya kuhamasisha wananchi wa Mkoa huo kuunganisha umeme katika nyumba zao.

Vilevile, aliwataka wananchi hao kuongeza shughuli za uzalishaji mali kama vile viwanda vidogo vinavyotumia umeme ili kuongeza idadi ya matumizi ya umeme ambao mwingi hupotea kwa kukosa watumiaji ilhali wakazi wengi hawana huduma hiyo.

Katika ziara yake hiyo, Waziri aliwasha umeme katika Kijiji cha Busomeke na kuwataka wananchi wa eneo hilo kuendelea kulipia shilingi 27,000 ili waunganishiwe umeme.

Akiwa katika Kijiji cha Mizanza, Dkt. Kalemani aliiagiza TANESCO, kuharakisha upelekaji wa nguzo kijijini hapo, ili kuwapa fursa wakazi wa kijiji hicho kuunganishiwa umeme.

Aidha, aliwataka wakazi hao kulipia gharama za uunganishwaji na kutandaza nyaya katika nyumba zao.

Aliendelea kusisitiza kuwa miradi ya usambazaji umeme vijijini haina fidia, hivyo wananchi watoe ushirikiano kwa wakandarasi na TANESCO pindi wanapopitisha miundombinu katika maeneo yao kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa kazi hiyo.

Hata hivyo, aliwataka kutumia wakandarasi walioainishwa na TANESCO na wanaotambulika katika serikali za mitaa na vijiji vyao ili kuepuka vishoka na watu wasio waaminifu.

Sambamba na hilo, aliwaeleza kuwa wasikubali kulipia miundombinu ya umeme kama nguzo, nyaya, mashineumba (Transfoma) wala mita za LUKU.

# MATUKIO PICHANI







*Watumishi wa Wizara ya Nishati wakipata elimu kuhusu ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya Corona. Mafunzo hayo yalifanyika katika Ofisi za Wizara zilizopo Mtumba na Kikuyu jijini Dodoma, Aprili 15 mwaka huu.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (katikati) akizungumza na viongozi wa Kijiji cha Mizanza, Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, alipofanya ziara ya kukagua shughuli za usambazaji umeme vijijini, Aprili 27, 2020.*



*Mbunge wa Manonga, Saif Gulamali (katikati) akizungumza na viongozi wa Kijiji cha Mizanza, Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, alipofanya ziara ya kukagua shughuli za usambazaji umeme vijijini, Aprili 27, 2020. Kulia ni Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani.*

# WAZIRI KALEMANI AWASHA UMEME MKALAMA



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akiwasha umeme kwenye Zahanati ya kijiji cha Mkalama, wilayani Mkalama, Mkoa wa Singida, Aprili 19, 2020 huku akishuhudiwa na viongozi wachache ikiwa ni hatua ya kuepuka mikusanyiko ya wananchi ili kujikinga na ugonjwa wa Corona.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa pili kulia) na Ujumbe wake, wakiangalia nguzo za umeme zilizorundikwa chini akiwa katika ziara ya kazi eneo la Kiomboi, Singida, Aprili 19 mwaka huu. Waziri aliagiza kuondolewa kwa nguzo hizo mara moja, zisimikwe na kuwaunganishia umeme wananchi wa eneo hilo.*

**Veronica Simba – Singida**

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani amewasha umeme katika maeneo kadhaa ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida na kusisitiza viongozi wa wilaya, vijiji na vitongoji kutoa kipaumbele kwa taasisi za umma zilizo katika maeneo yao ili ziunganishiwe nishati hiyo muhimu.

Akiwa katika ziara ya kazi wilayani humo, Aprili 19 mwaka huu, Dkt Kalemani alibainisha kuwa kipaumbele cha Serikali kupeleka umeme vijijini ni katika kuhakikisha taasisi zote za umma zinakuwa na umeme ili kuziwezesha kutoa huduma bora zaidi.

Alisema kuwa, Rais John Magufuli ametoa pesa nyingi kwa lengo la kupeleka umeme vijijini, hivyo ni lazima fedha hizo zitumike kwa busara katika kukidhi mahitaji ya wananchi walio wengi, hususan katika kuboresha huduma za afya, elimu, maji, kilimo pamoja na uanzishwaji viwanda vidogo vidogo.

"Ndugu zangu viongozi, nawasisitiza mhakikishe taasisi zote za umma katika maeneo yenu zinalipiwa gharama ya kuunganisha umeme ambayo kwa vijijini ni shilingi elfu 27 tu ili ziunganishiwe nishati hiyo na hivyo kuboresha huduma."

Akizungumza kwa nyakati tofauti na viongozi wa vijiji vya Milade na Mkalama baada ya kuwasha umeme katika Zahanati za vijiji hivyo, aliwapongeza kwa kuona umuhimu wa kulipia gharama za umeme zilizowezesha kuunganishiwa nishati hiyo na kuwataka viongozi wengine wa vijiji na vitongoji nchini kote kuiga mfano huo.

Katika hatua nyingine, Dkt Kalemani alitoa muda wa siku saba kwa Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, wilayani Iramba, kuvuta nyaya na kuwaunganishia umeme wananchi katika

INAENDELEA UK. 20

# WAZIRI KALEMANI AWASHA UMEME MKALAMA

INATOKA UK. 19

kijiji cha Msingi.

Waziri alitoa agizo hilo baada ya kushuhudia nguzo zilizosimikwa kwa muda mrefu pasipo kufungwa nyaya wakati akipita eneo hilo akitokea Mkalama.

Alimtaka Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Jones Olotu ambaye alifuatana naye katika ziara hiyo kumchukulia hatua Mkandarasi husika endapo hatatimiza agizo hilo.

Aidha, akiwa eneo la Kiomboi, Waziri alitoa siku tano kwa Mkandarasi husika kuhakikisha anaondoa nguzo za umeme zilizorundikwa chini na kuzitumia kuwaunganishia umeme wananchi wa eneo hilo.

Akiwa ameoneshwa kukerwa na hali hiyo ya nguzo kurundikwa wakati wananchi wa eneo husika hawana umeme, Waziri alimwagiza Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mkoa wa Singida, Abdulahaman Nyeye kumchukulia hatua Meneja wa Shirika hilo wilayani Iramba, endapo atashindwa kusimamia utekelezaji wa agizo lake.

Pia, alimwagiza Mkuu wa Wilaya husika kumchukulia hatua za kisheria Mkandarasi husika endapo hatatekeleza agizo lake ikiwa ni pamoja na kumweka ndani.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Mhandisi Jackson Masaka, aliipongeza Serikali inayoongozwa na Rais John Magufuli kwa kutekeleza kikamilifu ahadi zake kwa wananchi, ikiwemo upelekaji umeme vijijini.

Naye Mbunge wa Jimbo hilo, Allan Kiula, alimpongeza Waziri wa Nishati na Naibu wake Subira Mgalu kwa kazi nzuri ya kusimamia utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini.

Vilevile, alimwomba Waziri Kalemani kufikisha salamu za shukrani kwa Rais Magufuli kutokana na upendeleo ambao amekuwa akiwapatia



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mbele-kulia) akiwa amefuatana na viongozi na watendaji mbalimbali wa Serikali wakati akikagua utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini wilayani Mkalama, Mkoa wa Singida, Aprili 19, 2020.*

katika kuwapelekea miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo umeme.

Hadi sasa jumla ya vijiji 57 vya Wilaya ya Mkalama kati ya 70 vilivyopo, vimekwishafikishiwa nishati ya umeme. Waziri Kalemani ameeleza kuwa hadi kufikia Juni 2021, vijiji vyote vitakuwa vimekwishapelekewa umeme.

Waziri Kalemani ameendelea kusisitiza kuwa katika kipindi hiki ambacho Taifa linakabiliana na ugonjwa wa Corona, ziara zake kukagua miradi katika maeneo mbalimbali hazitahusisha wananchi ili kuepuka mikusanyiko. Badala yake, ziara zitahusisha viongozi wachache wa vijiji na vitongoji katika maeneo husika.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akikata utepe kabla ya kuwasha rasmi umeme katika Zahanati ya Kijiji cha Milade, Wilaya ya Mkalama, Mkoa wa Singida, Aprili 19 mwaka huu. Wa kwanza kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Mhandisi Jackson Masaka na wa kwanza kulia ni Mbunge wa Mkalama, Allan Kiula.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kushoto), akitoa maelekezo kwa watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kumsimamia Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Umeme Vijijini wilayani Iramba, kufunga nyaya za umeme katika nguzo alizosimika katika Kijiji cha Msingi na kuwaunganishia umeme wananchi ndani ya siku saba. Alitoa agizo hilo Aprili 19 mwaka huu.*

# MATUKIO PICHANI



*Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Mhandisi Jackson Masaka (kulia) akitoa salamu za ukaribisho kwa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (anayesaini kitabu), baada ya Waziri kuwasili wilayani humo kwa ajili ya ziara ya kazi, Aprili 19 mwaka huu. Wa kwanza kushoto ni Mbunge wa Mkalama, Allan Kiula.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa kwanza kushoto), akisalimiana na viongozi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, alipowasili wilayani humo Aprili 19, 2020 kwa ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akitoa maelekezo kwa watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), alipokuwa katika ziara ya kazi wilayani Mkalama, Mkoa wa Singida, Aprili 19, 2020. Wa kwanza kushoto ni Mbunge wa Mkalama, Allan Kiula na wa pili kushoto ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Mhandisi Jackson Masaka.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mbele) na Ujumbe wake, wakiwa katika ziara ya kazi wilayani Mkalama, Mkoa wa Singida, Aprili 19 mwaka huu. Wa kwanza kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Mhandisi Jackson Masaka.*


Wizara ya Nishati

#NishatiTukoKazini

# HERI YA SIKUKUU YA WAFANYAKAZI 2020

***Tunachapa kazi kuhakikisha nishati tulizonazo zinawezesha maendeleo ya viwanda na ukuaji wa uchumi.***

## *JIKINGE NA UWAKINGE WENGINE DHIDI YA COVID 19 (CORONA)*



Wizara ya Nishati

Wizara_ya_nishati_tanzania

@nishati2017

Wizara ya Nishati

www.nishati.go.tz